TANGAZO LA SERIKALI NA. 79 la tarehe 2/7/2025

SHERIA YA WAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 60(3))*

NOTISI YA MIKATABA YA KIMATAIFA NA KIKANDA ILIYORIDHIWA YA USAFIRI MAJINI YA MWAKA 2025

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Mikataba ya Kimataifa na Kikanda Iliyoridhiwa ya Usafiri Majini ya Mwaka 2025.

Tafsiri

2. Katika Notisi hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"mikataba ya kimataifa na kikanda iliyoridhiwa" maana yake ni mikataba, itifaki, makubaliano mengine ya kimataifa au kikanda ambayo imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Ibara 63(3)(d) na (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mikataba ya kimataifa, itifaki, viambatisho na mikataba ya kikanda iliyoridhiwa

3. Mikataba ya kimataifa, itifaki, viambatisho na mikataba ya kikanda kuhusu masuala ya usafiri majini ambayo imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

MIKATABA YA KIMATAIFA, ITIFAKI, VIAMBATISHO NA MIKATABA YA KIKANDA KUHUSU MASUALA YA USAFIRI MAJINI ILIYORIDHIWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SEHEMU A: MIKATABA YA KIMATAIFA

1. Mikataba ya kimataifa kuhusu usafiri majini ifuatayo imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

(a) Mkataba wa Shirika la Bahari Duniani wa mwaka 1948;
(b) Mkataba wa Kimataifa wa Mistari ya Ukomo wa Kupakia wa mwaka 1966;
(c) Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Kipimo cha Uwezo wa Kusheheni wa Meli wa mwaka 1969;
(d) Mkataba wa Kimataifa wa Dhima ya Madai Kwa Madhara Yanayotokana na Uchafuzi wa Mafuta wa mwaka 1969;
(e) Mkataba wa Kimataifa Kuhusiana na Haki ya Kuingilia Kati Matukio ya Ajali Katika Bahari Kuu Yanayotokana na Uchafuzi wa Mafuta wa mwaka 1969;
(f) Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Kanuni za Kuzuia Ajali Baharini wa mwaka 1972;
(g) Mkataba wa Kuzuia Uchafuzi Baharini Yanayotokana na Utupaji wa Taka au Masuala Mengine wa mwaka 1972;
(h) Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa mwaka, 1974;
(i) Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Satelaiti za Usafiri Majini wa mwaka 1976;
(j) Mkataba wa Shirika la Satelaiti za Usafiri wa Majini la Kimataifa wa mwaka 1976;
(k) Mkataba wa Kimataifa wa Mafunzo, Uthibitisho na Uangalizi kwa Mabaharia wa mwaka 1978;
(l) Mkataba wa Kimataifa wa Upekuzi na Uokoaji Majini wa mwaka 1979;
(m) Mkataba Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Usafiri Baharini wa mwaka 1982;
(n) Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafu Kutoka Kwenye Meli wa mwaka 1973;
(o) Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo Vilivyo Kinyume na Usalama wa Usafiri wa Baharini wa mwaka 1988;
(p) Mkataba wa Kimataifa wa Utayari, Mwitikio na Ushirikiano Dhidi ya Uchafuzi wa Mafuta wa mwaka 1990;
(q) Mkataba wa Kimataifa wa Ajira za Baharini wa mwaka 2006;
(r) Mkataba wa Uwezeshaji wa Usafiri Majini wa mwaka 1965;
(s) Mkataba wa Nyaraka za Utambulisho wa Mabaharia wa mwaka 1958;
(t) Mkataba wa Kimataifa wa Kuunganisha Sheria Zinazohusu Hati za Usafirishaji Majini na Itifaki ya Saini (Kanuni za Hague) wa mwaka 1924; na

*Tangazo la Serikali Na. 79 (Linaendelea)*

(u) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Usafirishaji wa Bidhaa kwa Njia ya Bahari (Kanuni za Humbarg) wa mwaka 1978.

SEHEMU B: ITIFAKI ZILIZORIDHIWA

2. Itifaki za kimataifa kuhusu usafiri majini ifuatayo imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

(a) Itifaki ya Kuingilia Kati Matukio ya Uchafuzi Katika Bahari Kuu Unaotokana na Vitu Vingine Isipokuwa Mafuta ya mwaka 1973;

(b) Itifaki ya Kuzuia Vitendo Vilivyo Kinyume na Usalama wa Usafiri Majini na Majukwaa Yasiyohamishika yaliyo Katika Rafu ya Bara ya mwaka 1988;

(c) Itifaki ya Kurekebisha Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Dhima ya Madai Kwa Madhara Yanayotokana na Uchafuzi wa Mafuta ya mwaka 1992; na

(d) Itifaki ya Kuanzisha Mfuko wa Kimataifa wa Fidia za Madhara Yanayotokana na Uchafuzi wa Mafuta ya mwaka 1992.

SEHEMU C: VIAMBATISHO VYA KIMATAIFA VILIVYORIDHIWA

3. Viambatisho vya kimataifa kuhusu usafiri majini ifuatayo imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

(a) Kiambatisho I kuhusiana na Uzuiaji wa Uchafuzi wa Mafuta cha mwaka 1978;

(b) Kiambatisho II kuhusiana na Udhibiti wa Uchafuzi wa Vimiminika vyenye Sumu Vilivyo katika Shehena Zisizofungashwa cha mwaka 1987;

(c) Kiambatisho III kuhusiana na Uzuiaji wa Uchafuzi wa Vitu vyenye Madhara Vinavyosafirishwa Baharini Katika Vifungashio cha mwaka 1992;

(d) Kiambatisho IV kuhusiana na Uzuiaji wa Uchafuzi Unaotokana na Majitaka Kutoka Kwenye Meli cha mwaka 2003; na

(e) Kiambatisho V kuhusiana na Uzuiaji Taka Kutoka Kwenye Meli cha mwaka 1988.

SEHEMU YA D: MIKATABA YA KIKANDA

4. Mkataba wa Afrika wa Usafiri Majini wa mwaka 1994 ni Mkataba wa kikanda kuhusu usafiri majini ambao umeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dodoma,
20 Januari, 2025

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Uchukuzi*